JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAASISI YA UONGOZI

UONGOZI Institute

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## TAASISI YA UONGOZI KUFANYA KONGAMANO LA KWANZA LA WAHITIMU WAKE

**1 Agosti 2025, Dar es Salaam:** Kongamano la kwanza la wahitimu wa Taasisi UONGOZI litafanyika leo katika ukumbi wa mikutano wa Hoteli ya Serena. Mgeni Rasmi wa Tukio hili atakuwa **Eng. Zena Ahmed Said**, Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

Wasilisho kuu litatolewa na Bw. Omari Issa, Mkuu wa Chuo cha Afrika cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela.

Wahitimu hawa ni wale waliomaliza programu za mafunzo ya muda mrefu zitolewazo na Taasisi: Stashahada ya Uzamili ya Uongozi (*Postgraduate Diploma in Leadership*), Programu ya Uongozi Ngazi ya Cheti (*Certificate in Leadership*), na Programu ya Uongozi kwa Wanawake (*Women's Leadership Programme*). Kongamano hili litakuwa ni mwanzo wa jitihada za kimakusudi za kuhamasisha mchango wa kundi hili katika utekelezaji wa programu za Taasisi. Dhima ni *"Nafasi ya wahitimu wa Taasisi ya UONGOZI katika kuleta uongozi wa kimageuzi barani Afrika".*

Lengo la programu hizi ni kujenga na kuimarisha uwezo wa viongozi katika maeneo matatu: sifa binafsi za uongozi, usimamizi wa rasilimali watu, na uongozi wa taasisi. Zimeandaliwa kwa ajili ya viongozi wanaotaka kujiendeleza bila kukwamisha kazi yao. Wakufunzi wa programu ni wataalamu wabobezi katika masuala ya uongozi kutoka nchi mbalimbali duniani.

Stashahada ya Uzamili ya Uongozi na Programu ya Uongozi Ngazi ya Cheti zimeandaliwa na kutolewa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto cha Mafunzo ya Utawala, kilichopo nchini Finland. Utekelezaji wa programu hizi mbili unawezeshwa kwa kiasi kikubwa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Finland. Programu ya Uongozi kwa Wanawake inafadhiliwa na Serikali hizo mbili pamoja na Umoja wa Ulaya.

Ushiriki katika tukio hili ni kwa mwaliko pekee.

Imetolewa na,

Suzana Aroko

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma**

Kiwanja Na. 100, 1 Barabara ya Magogoni, Kivukoni. S.L.P. 105753, 11101 Dar es Salaam. Simu: +255 22 211 0372/3. Nukushi: +255 22 211 0374. Barua pepe: barua@uongozi.go.tz. Tovuti: www.uongozi.go.tz.